**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**
**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA PILI**
**(OKTOBA - DESEMBA, 2024/25) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA LEWIS KALINJUNA**
**TAREHE 06-7.02.2025**

## A. WAJUMBE

**WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Elias R. Masumbuko | Mstahiki Meya (Mwenyekiti) |
| 2. | Ndg. Revocatus Lutunda | Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) |
| 3. | Mhe. Zamda S. Mwebea | Naibu Meya |
| 4. | Mhe. James M. Matinde | Mjumbe |
| 5. | Mhe. John P. Kisandu | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Picca N. Chogero | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Sheilla D. Mshandete | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Victor T. Mmanywa | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Moshi H. Kanji | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Hassan R. Mwendapole | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Msabila M. Kulwa | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Zuhura Waziri | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Juma M. Nkwabi | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Reuben N. Kitinya | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mussa E. Andrea | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mariam L. Nyangaka | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Paschazia C. Seni | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Peter J. Kwoliba | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Victor Y. Mkwizu | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Esther F. Makune | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ezekiel J Sabo | Mjumbe |
| 22. | Mhe.Enock C. Lyeta | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Reuben M. Dotto | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Gulamhafeez Mukadam | Mjumbe |

## B. WASIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Patrobas Katambi (MB) | Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Lucy Mayenga (Mbunge VM) | Kwa taarifa |

**C. WATAALAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pius M. Sayayi | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu. |
| 2. | Kuchibanda K. Snatus | Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira. |
| 3. | Charles Luchagula | Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni, Michezo na Vijana |
| 4. | Mensaria Mrema | Mkuu wa Divisheni ya Mipango na uratibu |
| 5. | James Mashindike | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |
| 6. | Lenard Chepe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 7. | Eng Boaz Kayira | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, maendeleo ya Vijiji na Miji. |
| 8. | CPA Peter Tarimo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 9. | Salome Komba | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii. Mazingira. |
| 10. | Mary S. Maka | Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 11. | Lucas Mzungu | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari. |
| 12. | Octavina Kiwone | Mratibu TASAF |
| 13. | Jacob Mwinuka | Afisa Ardhi Mteule wa Ofisi ya Ardhi Manispaa. |
| 14. | Simon Shoo | Kny ya Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 15. | Dr Elisha Robert | Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe. |
| 16. | Edith Mwijage | Kny: Mthibiti Ubora wa Shule. |
| 17. | Caroline Mzelu | Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi |
| 18. | CPA Kishenyi Mulokozi | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 19. | Adv. Rose Matunda | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria. |
| 20. | CPA Sunday Nkwambi | Mhasibu wa Matumizi |
| 21. | Ezra Manjerenga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira |
| 22. | Michael Makotwe | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Usimamizi na Ufuatiliaji |
| 23. | Jesca Kipingu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini |
| 24. | Edwin Kagugu | Mhasibu wa Mapato |

**D. WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe Julius Mtatiro | - | DC |
| 2. | Said Kitinga | - | DAS |
| 3. | CPA. Eng Andrew Kifua | - | For RAS |
| 4. | ASF Fatma Sato | - | DFO |
| 5. | A/INSP Jastin Nyatano | - | OCD |
| 6. | Lt CoL Ford Mwakasege | - | MJA |
| 7. | ASI- Elizabeth G. Kaka | - | Ag. DIO |
| 8. | SP Deogratius Sinyinza | - | Ag. DPO |

9. COL Boniventura Mnimbo - B/COMD
10. Mohamed Doo - AG. DBC
11. Justine Kakuru - AG DSO
12. Baraka Bulongo - LGO
13. Anold Makombe - M/Kiti CCM (W)
14. Hamisa S. Chacha - Katibu CCM (W)
15. Samwel Jackson - Katibu wa Mbunge

**E. WAKUU WA TAASISI**

1. Kimonga Joseph - TEMESA
2. Sebastian Yohana - TANESCO
3. Eng. Kulwa E. Maige - TARURA
4. Eng. Uswege Musa - SHUWASA

**F. WATENDAJI WA KATA**

1. Levania Mliliye - Mtendaji wa Kata ya Ngokolo
2. Fortunatus L. Jilala - Mtendaji Kata ya Kitangili
3. Andrew Katabalo - Mtendaji wa Kata ya Kolandoto
4. Adella Mukinga - Mtendaji wa Kata ya Kizumbi
5. Joshua Masengwa - Mtendaji wa Kata ya Ndala
6. Ibrahim Inyasi - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Old Shinyanga
7. Elizabeth Mbate - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Masekelo
8. Mahiba Pastory - Mtendaji wa Kata ya Lubaga
9. Mafuru P. Mafuru - Mtendaji wa Kata ya Mwawaza
10. Simon Mashishanga - Mtendaji wa Kata ya Mjini
11. Stella Herman - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata
12. Mayala Ibrahim - Mtendaji wa Kata ya Chamaguha
13. Michael Joshua - Mtendaji wa Kata ya Mwamalili
14. Jacquiline Nkwaje - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kambarage
15. Emilini Mtambo - Mtendaji wa Kata ya Ndembezi
16. Irene Mshandete - Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli
17. Ponsian Ngodita - Mtendaji wa Kata ya Chibe

**F: AFISA TARAFA**

1. Telezia K. Alois - Afisa Tarafa ya Mjini
2. Gregory Kachira - Afisa Tarafa ya Ibadakuli
3. Neema Mukandala - Afisa Tarafa ya Old Shinyanga

**G: WAANDISHI WA HABARI.**

1. Marco Maduhu - NIPASHE
2. Kareny Masasy - Habari Leo
3. Mwamvita Issa - TVE

4. Abel Michael - Wasafi Media
5. Flora Masalu - Global TV
6. Elias Gamaya - Afisa Habari Shinyanga Manispaa
7. Daniesa Malula - Malula TV
8. Stella Ibengwe - Mwandishi Jambo FM

**SEKRETARIETI**

1. Esther Daudi Mwandishi wa Vikao (CC)
2. Damaris Charles Mwandishi wa Vikao (CC)
3. Amina Juma Mwandishi Mwendesha Ofisi (MMO)

**Agenda za mkutano zitakuwa kama ifuatavyo:-**

**Siku ya kwanza tarehe 06.02.2025**

1. Kufungua mkutano
2. Kuthibitisha agenda za mkutano.
3. Kupokea na kujadili taarifa za kwenye Kata kutoka kwa Madiwani wa Kata husika Pamoja na majibu ya changamoto za Kata kwa kipindi cha robo ya Kwanza.
4. Kuahirisha mkutano.

**Siku ya pili tarehe 07.02.2025**

5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Baraza la Madiwani wa kawaida wa tarehe 31- 01.10.2024.
6. Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025
   - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 15.10.2024
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 16.10.2024.
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe17.10.2024.
   - Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 24.10.2024,19.11.2024 na 19.12.2024
7. Kupokea taarifa za utekelezaji wa Divisheni mbalimbali za Kamati za kudumu kwa robo ya pili 2024/2025.
   - Kamati ya kudhibiti UKIMWI
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
   - Kamati ya Fedha na Utawala
   - Taarifa ya ziara ya Kamati ya fedha na Utawala ya (Oktoba-Disemba 2024) iliyofanyika tarehe 24.01.2025
8. Taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa.
9. Kufunga kikao.

**AGD Na.01:2024/25** **MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

**Kumb: BAR.02.1.1** Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kupitia taarifa ya robo ya pili 2024/2025 Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kuuliza maswali ya papo kwa papo.

**Kumb: BAR.02.2.2** Wajumbe waliuliza Maswali yaliulizwa kama ifuatavyo**:-**

**SWALI:** Je ni lini Halmashauri itakamilisha kituo cha Polisi Ngokolo ili kuunga mkono juhudi za Wananchi?

**JIBU:** Kwa kuwa Halmashauri inaendelea na mchakato wa bajeti, Barua ilipokelewa ya kuomba kuwasilisha maboma yote ya vituo vya polisi, hivyo itatengwa bajeti ya kukamilisha maboma hayo.

**SWALI:** Ni lini Halmashauri itakamilisha ujenzi wa kituo cha Afya Kata ya Ndembezi?

**JIBU:** Maboma hayo yamewekwa kwenye mpango wa bajeti, Hata hivyo wakatii mchakato wa bajeti unaendelea barua imeletwa ya kuitaka Halmashauri kuwasilisha Maboma yote yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi hivyo yamewasilishwa kwa kusubiri utekelezaji.

**SWALI:Ni lini Wananchi wa Kata ya Mwamalili watapimiwa Viwanja**

**JIBU:** Suala la upimaji linaanza na uhitaji, hivyo wananchi wakae kupitia WDC ili waombe kupimiwa (muhtasari uwasilishwe Halmashauri kwa ajili ya kupimiwa).

**SWALI:** Ni lini Wananchi (9) wa Butulwa Kata ya Old Shinyanga watalipwa fidia **Sh 33,000,000/=**

**JIBU:** Mwaka wa fedha 2024/2025 ilitengwa fedha **Sh 70,000,000/=** kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Hivyo suala hili litaingizwa kwenye bajeti ya 2025/2026.Aidha, wananchi ambao hawajalipwa fidia wataendelea kutumia maeneo hayo mpaka watakapolipwa fidia.

Wajumbe walipokea majibu ya ufafanuzi na kuelekeza mambo yafuatayo yafanyiwe kazi**;**

**MAAZIMIO:**

- Menejimenti ifanyie kazi Suala la ulipaji wa fidia eneo la Butulwa na kuwasilisha taarifa katika Kamati husika.
- Kuongea na wananchi wa eneo hilo ili waendelee kutumia maeneo yao mpaka fidia itakapolipwa.

**SWALI:** Ni lini Stendi ya Magari ya kuelekea Mwawaza itaanza kufanya kazi ili kupunguza adha ya usafiri kwa wananchi.

**Wajumbe walijadili suala hili na kuazimia ifuatavyo:**
**AZIMIO:**
Menejimenti ifanyie kazi suala la uanzishaji wa Stendi ya magari ya kuelekea Kata ya Mwawaza na kuwasilisha taarifa katika Kamati husika.

**AGD Na.01:2023/24** **KUFUNGUA MKUTANO**

**Kumb: BAR.02.1.1** Mwenyekiti alifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya pili saa 05.12 Asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe, Wataalam, Kamati ya ulinzi, Waandishi wa Habari na Wananchi katika Mkutano huo.

**AGD Na.02: 2023/24** **KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 07. 02. 2025.**

**Kumb: BAR .02.2.1** Jumla ya agenda 09 zilithibitishwa kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani kuwa agenda halali za Mkutano.

**AGD Na.03 :2023/24:** **KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KWENYE KATA KUTOKA KWA MADIWANI WA KATA HUSIKA.**

**Kumb: BAR.02.3.1** Wajumbe waliwasilisha taarifa za Kata 17 kwa kuelezea mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo katika Kata zote. Ilielezwa kuwa changamoto nyingi katika Kata zinajirudia hivyo inahitajika kupata utatuzi wa kudumu. Pamoja na changamoto zilizowasilishwa zilizoonekana na kuainishwa katika Kata zote ni kama ifuatazo;

- Ulipaji wa fidia katika maeneo mbalimbali.
- Upungufu wa matundu ya Vyoo katika baadhi ya Shule
- Kutokamilika kwa miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Kata.
- Upungufu wa Wataalam wa Kada mbalimbali katika Kata.
- Ubovu wa Miundombinu ya Barabara hususani Barabara za Mitaa

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipongeza Menejimenti kwa kutatua changamoto nyingi katika Kata.
Hata hivyo wajumbe walihitaji ufafanuzi kwa hoja zifuatazo;

**Hoja kuhusu kutoa elimu ya ufugaji kwa wananchi.**
Wajumbe walieleza Halmashauri ijielekeze kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ufugaji wa ndani ili kudhibiti mifugo wanaozurura na kufanya uharibifu wa mazao na miti iliyopandwa.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Suala hili linaendelea kufanyika Halmashauri inaelimisha wafugaji kupitia maafisa Ugani walioko katika ngazi ya kata. Hata hivyo barua imeandikwa kwa Watendaji wa Kata kuwataka kusimamia utekelezaji.

**Hoja kuhusu upungufu wa Watendaji, Kata ya Chibe Mtaa wa Mwalugoye.**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Serikali imeajiri Watendaji wa Kata na Mitaa na kuhakikisha hakuna Mtaa ambao hauna Mtendaji isipokuwa waliopo masomoni.

**Hoja kuhusu kuweka matuta kwenye barabara ya Nguzo nane ili kuzuia ajali kutokea.**
Wajumbe walihitaji kujua ni lini matuta yatawekwa katika Barabara hiyo ili kuzuia ajali.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa taasisi inayohusika na suala hili hawakuhudhuria baraza Suala hili litafanyiwa kazi na majibu yatawasilishwa katika Kamati husika.

**Hoja kuhusu kuchonga na kufungua barabara**
**Wajumbe walihitaji kujua ni lini Barabara hizo zitachongwa**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Ofisi inaendelea kujipanga ili kupeleka fedha za uchongaji wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Hoja kuhusu mtandao wa maji Kata ya Lubaga**
Wajumbe walitoa hoja kuwa Kata ya Lubaga ilipewa Kilometa moja ambayo ni ndogo hivyo ufanyike utaratibu wa kupeleka huduma hiyo.

Hoja kuhusu kukosekana shule Shikizi Kata ya Masekelo utaratibu wa kupata kibali cha uanzishaji wa shule uharakishwe ili kupunguza adha kwa wanafunzi.

**Kumb: BAR.02.3.2**

**Hoja kuhusu kupeleka walimu mbadala Shule ya Sekondari Lubaga.**
Wajumbe walihitaji kujua utaratibu uliopo wa kupeleka walimu mbadala katika shule hiyo baada ya kuhamisha baadhi ya walimu.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, Lubaga Sekondari Walimu waliohamishwa tayari walimu mbadala wamepelekwa ili kuziba nafasi hizo)
Wajumbe walipokea Maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa na wataalam.

Baada ya majadiliano wajumbe walisisitiza kuwa Wakuu wa taasisi wapokee changamoto zinazowahusu na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Katibu aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kuwasilisha mafanikio na changamoto kutoka katika Kata zao na alieleza kuwa Changa moto zote zilizowasilishwa zinafanyiwa kazi kwa kuwa miradi mingi inaendelea kutekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani

husususani ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika Shule za msingi na Sekondari.

**AGD Na.04 :2023/24:** **KUAHIRISHA MKUTANO**

Kikao cha kujadili taarifa za Kata kiliahirishwa saa 07:27 mchana

**SIKU 2** **07. 01. 2025**

**AGD Na.05:2023/24:** **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 31. 10. 2024 - 01.11.2024.**

**Kumb: BAR.02.5.1** Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe **31. 10. 2024 - 01.11.2024** ulisomwa ukurasa kwa ukurasa na wajumbe kuridhia kuwa yaliyomo ndiyo yaliyojadiliwa na hivyo ulithibitishwa na kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo.

**AGD Na.06:2024/25:** **KUPOKEA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA KWANZA 2024/2025.**

**Kumb: BAR.02.6.1** Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya pili ya mwaka 2024/2025 ambayo tayari ilithibitishwa katika vikao vya Kamati vilivyofanyika,

- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 15.10.2024
- Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 16.10.2024.
- Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe17.10.2024.
- Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 24.10.2024,19.11.2024 na 19.12.2024.

**Kumb: BAR.02.6.2** Wajumbe waliipokea Mihtasari ya Kamati za kudumu na kuridhia kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

**AGD Na.07:2023/24:** **KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA DIVISHENI MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA KWANZA 2024/2025**.

**Kumb: BAR.02.7.1** Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Divisheni na Vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambazo ni Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu, Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ya Fedha na Utawala kwa robo ya pili 2024/2025 iliwasilishwa kwa Wajumbe kama ifuatavyo;

**Kumb: BAR.02.7.2** **Kamati ya Kudhibiti UKIMWI**

Taarifa hii iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa, Shughuli za kudhibiti Ukimwi zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni shughuli zisizo za tiba na shughuli za tiba. Ilielezwa kuwa katika kipindi cha

robo ya pili ya Oktoba hadi Disemba, 2024 shughuli mbalimbali zilitekelezwa.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuipitisha

**Kumb: BAR.02.7.3** **Kamati ya Mipango Miji na Mazingira**

Taarifa ya Mipango miji na Mazingira iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa katika kipindi cha robo ya pili ya Oktoba – Disemba, 2024/2025 Vitengo vilivyo chini ya Divisheni ya Miundombinu na maendeleo ya Vijiji na Miji inayohusisha Vitengo vya ujenzi, Mazingira na Ofisi ya Ardhi na Mipango vilitekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

**Kumb: BAR.02.7.4** **Hoja kuhusu usimamizi wa usafi na udhibiti wa Taka.**

Wajumbe walieleza kuwa kazi ya udhibiti wa taka isimamiwe ipasavyo wananchi waelekezwe kufanya usafi Maafisa Afya, Watendaji wa Kata na Mitaa watimize majukumu yao ili Halmashauri iendelee kupata Tuzo.

Aidha Mzabuni anayekusanya taka asaidiwe kwa kuwaelimisha wananchi kulipia fedha ya uzoaji taka.

Kamati ilipokea ushauri na kueleza kuwa Halmashauri imejipanga kupitia vikao vyake kuimarisha usimamizi wa usafi kwa kuwahimiza Watendaji kupita mitaani pia kuwatangazia wananchi kwa kutumia vyombo vya matangazo (PA).

**Kumb: BAR.02.7.5** **Hoja kuhusu kununua silaha za kuuwa Wanyama wanaosumbua Jamii (Wanyama wakali)**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa mpango wa kupata kibali cha kununu na kutumia silaha ili kudhibiti Wanyama hao upo ili kuondoa adha ya kutumia Askari wa kuazima katika Mikoa mingine.

**Kumb: BAR.02.7.6** **Hoja kuhusu kuongeza bajeti ya kuchonga barabara ili kuwasaidia TARURA kwa kuwa bajeti yao ni ndogo**.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri itaanza zoezi la uchongaji wa barabara kuanzia mwezi wa nne baada ya mvua kupungua, hivyo maeneo mengi yatafikiwa.

**Kumb: BAR.02.7.7** **Taarifa ya Uchumi, Afya na Elimu.**

Taarifa ya Uchumi, Afya na Elimu iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza cha kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba, 2024 kamati ya Uchumi, Afya na Elimu imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya kikao chake cha tarehe 21.01.2025 kilichojikita kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizofanyika katika Divisheni na Vitengo zilizo

chini ya kamati hii ambazo ni Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Elimu ya Awali na Msingi, Elimu ya Sekondari, Mipango na Uratibu, Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Divisheni ya Viwanda, Biashara na uwekezaji pamoja na kitengo cha Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Taarifa iliwasilishwa na kujadiliwa.

**Kumb: BAR.02.7.8** **Hoja kuhusu Kitengo cha Sanaa na Michezo**

Wajumbe walieleza kuwa Halmashauri iwekeze kwenye michezo na sio kuachia wadau, jitihada zifanyike Timu ziwepo.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kamati zitaendelea na ufuatiliaji na kuhakikisha suala la michezo linazingatiwa Aidha,Kitengo kinaendelea kuratibu shughuli za michezo ikiwemo mazoezi ya viungo, hivyo awamu ijayo waheshimiwa Madiwani watashirikishwa hata hivyo timu zinaendelea kuimarishwa.

**Kumb: BAR.02.7.9** **Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala.**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala iliwasilishwa ambapo wajumbe waliipongeza Kamati hiyo kwa shughuli wanazozifanya.

**Kumb: BAR.02.7.10** **Hoja kuhusu watumishi wa Halmashauri kuhama**

Wajumbe walihitaji kujua sababu inayopelekea Watumishi kuhama

Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala la watumishi kujiombea uhamisho, ni suala la Kisheria pia ni haki ya Watumishi kwani wameruhusiwa kuhama ili kufata wenza wao.

**Kumb: BAR.02.7.11** **Wajumbe walihitaji kujua ni Mpango upi uliopo ili kupunguza tatizo la Rasilimali watu ifikapo Juni, 2025.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Serikali inaajiri Watumishi kulingana na uhitaji na hata hivyo taarifa inaonesha kuwa upungufu mkubwa upo upande wa Walimu, kwa sasa Serikali imeajiri Walimu ambao wakipangiwa majukumu uhitaji utapungua.

Wajumbe walipokea majibu ya utekelezaji na kutoa pongezi  Kitengo cha Sheria kwa kazi nzuri wanazofanya kwa kusimamia mashauri Mahakamani.

**Kumb: BAR.02.7.12** **Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha na Utawala ya (Oktoba - Disemba 2024 iliyofanyika tarehe 24.01.2025**
**Hoja kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Sekondari ya Igalukilo-Kizumbi**

Wajumbe walieleza kuwa katika mradi huo Mkandarasi amechukua kazi nyingi hali inayopelekea kuchelewa kukamilisha mradi, je ni lini ujenzi utakamilika ili shule ianze kufanya kazi

Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala hili lilionekana wakati wa ziara na kwa kuwa Kazi hiyo ilitangazwa kwenye mfumo wa NEST mkandarasi huyo aliomba kwa kutumia majina tofauti akapewa pasipo kutambua kuwa ana kazi nyingine hivyo iliamuliwa aondolewe kwa kuwa anafanya kazi kwa kasi ndogo, taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kukamilisha kazi zinaendelea.

**AGD Na.08:2024/25:** **TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI.**
**Kumb: BAR.02.8.1** **Taarifa iliwasilishwa kwa kuwajulisha wajumbe mambo yafuatayo;**

i. Mapokezi ya fedha Sh 1,100,000,000.00 (bilioni moja 1,000,000,000.00 ujenzi wa jengo la Utawala na 100,000,000.00 kwa ajili ya kununua Dawa na vifaa Tiba.
ii. Taarifa ya utoaji wa chanjo iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa kampeni ya chanjo ya mifugo kitaifa kwa Ng’ombe,Mbuzi,Kondoo na Kuku Katika Halmashauri zote za Tanzania.
iii. Taarifa ya Matokeo ya mitihani kwa Shule za Sekondari na Msingi kwa kueleza ufaulu wa wanafunzi wa Darasa la saba, kidato cha pili na kidato cha nne.
iv. Taarifa ya utoaji mikopo kwa Vikundi vya wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Wajumbe walitoa pongezi kwa Wakuu wa Divisheni za Elimu Msingi na Sekondari kwa kufanya kazi nzuri na kuelekeza wapewe motisha ya kazi nzuri.
Baada ya majadiliano wajumbe waliazimia kuwa;

**Kumb: BAR.02.8.2** **AZIMIO:**
Wakuu wa Divisheni za Elimu msingi na Sekondari wapewe motisha kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia masuala ya elimu na kupandisha ufaulu wa wanafunzi.

**(i) Taarifa za Taasisi**

**(a) TARURA**

Taarifa ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ya matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kipindi cha robo ya pili iliwasilishwa na kujadiliwa.

**Ni lini barabara ya kutoka lami kwenda Hospitali ya Kolandoto itafanyiwa matengenezo.**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Barabara ya kutoka lami kwenda Hospitali ya Kolandoto imewekwa kwenye bajeti ya 2025/2026.

**Ni lini barabara ya Masekelo kutoka 'Centre' kuelekea Shule ya Sekondari Masekelo itachongwa.**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Barabara ya kutoka 'Center' kwenda Sekondari na Masekelo imewekwa kwenye bajeti ya **2025/2026.**

**Ni lini Barabara ya Ilwelyangula itafanyiwa matengenezo**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Barabara ya Ilwelyangula imeingizwa kwenye bajeti ya 2025/2026

**Ni lini vifusi vitaondolewa kwenye Daraja Barabara ya Chibe-Negezi na kufunika Calvati eneo la Mwamapalala**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Barabara ya Chibe – Negezi Mkandarasi hajalipwa kwa kazi hiyo hivyo atarudi kukamilisha mapungufu na kufanya kazi zote zilizobaki.

**Ni lini matengenezo ya Barabara ya Ibadakuli kuelekea uzogole itafanyiwa matengenezo**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa Barabara ya Ibadakuli – Uzogole kwa kuona umuhimu wake imeingizwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuwa imechimbika sana.

**Ni lini barabara ya Ndala Mwawaza itajengwa kwa kiwango cha Lami**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa barabara mradi huu utatekelezwa na Benki ya Dunia na taratibu za kuanza utekelezaji zinaendelea.

Aidha, Mhandisi alishauri kuwa Barabara za TASAF zikabidhiwe TARURA ili zifanyiwe matengenezo sababu zinasababisha ajali kwa jinsi zilivyoharibika.

Baada ya majadiliano wajumbe walishauri kuwa katika kazi zinazoendelea matengenezo ya dharula yafanyike kwenye Daraja la (Shinyanga – Kishapu).

**(b) TANESCO**

Taasisi hii haikuwa na taarifa ya maandishi ya kuwasilisha kwa wajumbe hivyo mwenyekiti aliruhusu wajumbe waulize maswali na kuwasilisha changamoto ambazo zitawasilishwa TANESCO na majibu yatawasilishwa katika mkutano wa Baraza

Aidha, wajumbe walieleza kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya kuangalia namna TANESCO watakavyoweza kuwasilisha/kuwajibika Halmashauri ili kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zinazowasilishwa na Waheshimiwa Madiwani kutoka kwa wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

**(c)SHUWASA**

Taarifa kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Maningira Shinyanga (SHUWASA) iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa mamlaka hiyo inahusika na utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Aidha Mamlaka ya majisafi na usafi wa Mazingira Manispaa ya Shinyanga inatekeleza gharama za miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka mwa fedha 2025/2026 ikiwa ni pamoja na; - Bajeti kuu ya Wizara ya maji kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa, Ruzuku itakayotokana na kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa mtambo wa kutibu tope kinyesi (FSTP) chini ya IFF-OBA Programme na Mapato ya ndani ya Mamlaka

Baada ya taarifa kupokelewa na kujadiliwa, Wajumbe walieleza kuwa Miundombinu ya maji inayowekwa izingatie maeneo yaliyopimwa (viwanja)
Aidha, wakati wa kuchimba mitaro ichimbwe mirefu ili kuweka uhifadhi wa mabomba.

**AGD Na.09:2023/24:** **KUFUNGA MKUTANO**

**NASAHA ZA VIONGOZI**

**Kaimu katibu Tawala ‘M’**

- Suala la TANESCO Meneja wa TANESCO afike na Kuiwasilisha taarifa Manispaa, pia wakati wa utekelezaji ushirikishwaji ufanyike ili kubaini maeneo yenye uhitaji zaidi.
- Suala la CHF iliyoboreshwa Mkuu wa Disheni ya Afya kufanya mawasiliano katika ngazi ya Mkoa ili kufanya utatuzi kuhusu madai ya fedha za iCHF.
- TARURA - Kuhuisha vibao viweze kusomeka ili wananchi wawe na uelewa.

**Katibu Tawala Wilaya**

- Alielezea kuhusu suala la kuua Wanyama wakali 'operation' ifanyike kwa kutumia silaha za sehemu nyingine.
- Kushughulikia malalamiko ya wananchi kwa kushirikiana na Watendaji ngazi ya Kata na Mitaa ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao.
- Wakuu wa Taasisi waitwe kwenye vikao vya WDC ili kutatua baadhi ya changamoto katika ngazi ya chini.

**Mkuu wa Polisi 'W'**

Wananchi waelekezwe kutoa taarifa ya matukio yanayotokea mtaani ili hatua zichukuliwe mapema.

**Katibu wa CCM Wilaya**

- Manispaa kufungua barabara ili zikabidhiwe TARURA
- Kushukuru Taasisi za Serikali kwa kazi nzuri ila waongeze ushirikishaji wakati wa utendaji

**Mstahiki Meya**

Kuwashukuru wajumbe kwakushiriki vema kwenye kikao

- Kuendelea kusimamia usafi wa mazingira
- TARURA kufanya matengenezo barabara ya Ugweto na Ilwelyangula.
- Kufanyia kazi barabara zilizotekekelezwa na mradi wa TASAF ili zikabidhiwe TARURA
- Taasisi za SHUWASA na TANESCO Kutoa kipaumbele kwa kupeleka huduma Kijiji cha Mwamapalala.

Baada ya nasaha na pongezi kutoka kwa Viongozi, Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 11:09 Jioni kwa kuwashukuru Wajumbe, waalikwa, Waandishi wa Habari, Wananchi pamoja na Wataalam kwa kushiriki vizuri Mkutano wa Baraza la Madiwani.

**KUMBUKUMBU HIZI ZIMETHIBITISHWA NA**

| | |
|---|---|
| ________________________ | ________________________ |
| Mwl Alexius R. Kagunze | Mhe. Elias R. Masumbuko |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE**________________